Tofauti zinazoletwa na hali ya uchumi je? Watu wenye hali nzuri ya kiuchumi aghalabu hujiona ni bora kuliko wale wa hali ya chini. Hii ni fikira ya hivi karibuni tu kwani katika maisha ya kimila ya kiafrika hapo zamano utajiri wa mtu haukumfanya ajione bora au awe na mamlaka juu ya wenzake. Juu ya hayo watu wote waliangaliwa na kushiriki katika kila shughuli pamoja na kwa faida ya kila mtu.

Sasa tuangalie jambo la mwisho, yaani kubaguliwa kwa wanawake. Swala hili la ubaguzi kwa wanawake ni tatizo la ulimwengu mzima na huzuka takribani katika kila kabila au taifa.

Tukipeleleza tutaona kuwa katika makabila mengi, wanawake wako katika hali ya chini. Mfano mmoja pengine utadhihirisha hali hii vyema. Uchunguzi umehakikisha kwamba ukiangalia idadi ya wakulima katika baadhi ya nchi za kiafrika utaona kuwa kuna wanawake wengi kuliko wanaume lakini wanawake hawana usemi au mamlaka yoyote katika kuendesha uchumi wa kilimo; wanofaidi ni wenye mashamba ambao wengi wao ni wanaume.

Basi tunaweza kusema kuwa maendeleo katika nchi yoyote hayatakuwa yakipatikana ikiwa watu wake watakuwa wakibaguana kwa ajili ya rangi, utamaduni, hali ya uchumi na hali ya maumbile yao yaani kwa kuwa ni wanawake au wanaume.

MASWALI

a) Eleza misingi ya ubaguzi duniani.

(alama 4)

b) Utamaduni, kulingana na taarifa hii, una maana gani? (alama 2)

c) Hivi leo katika mataifa mengi, ubaguzi hutokana na hali ya kiuchumi kwa kiwango kikubwa. Fafanua. (alama 2)

d) Kwa maoni yako, eleza sababu za mwanamke kubaguliwa hasa katika jamii nyingi za Kiafrika. (alama 3)

e) Eleza athari ya ubaguzi katika nchi za Kiafrika. (alama 2)

f) Toa maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika taarifa. (alama 2)

i) Ubaguzi

ii) Masalia

2) MUHTASARI

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa. Inakera mto kwa vitendo vya kigaidi. Inagadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba magaidi hawa wameelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani, damu ya mwananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini, vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao. Lakini cha kusikitisha ni kuwa, mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya misako inayoishia kuwanasa kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hii ya misako imeishia kunaswa raia wengi wasio na makosa. Wanaponaswa hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, mbinu hii yaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

MASWALI

- a) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi (alama 7, 1 utiririko)
(maneno 60-70)

Matayarisho:

Nakala safi

b) Kwa kutumia maneno yasiozidi 50 fupisha aya mbili za mwisho alama 6, 1 utiririko)
Matayarisho:

c) Nakala safi

MATUMIZI YA LUGHA

- a) Taja sauti iliyo na sifa zifuatazo (alama 1)
- i) Mbele, tandazwa, wastani _____
 - ii) Kikwamizo cha kaaka laini _____
- b) Ainisha mofimu katika neno hili (alama 2)
- Waoao

- c) Akifisha; (alama 3)
- hivyo ndivyo tunavyoweza kufikia vision 2030 wewe waonaje

- d) Eleza miundo miwili ya nomino katika ngeli ya U – I (alama 2)

- e) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizoko kwenye mabano (alama 2)

- i) Choka (tendea) _____
- ii) Ja (tendewa) _____

- f) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao (alama 3)
- N+H+N+Ts+T+N

- g) Changanua sentesi ifuatayo kwa kutumia jedwali (alama 3)
- Mkufunzi hodari amepita mtihani rahisi.

h) Kanusha sentensi;
Kuliko na njaa kwahitaji msaada

(alama 2)

i) Unda nomino kutokana na vitenzi ulivyopewa bila kutumia 'ku' katika uundaji wako (ala. 2)

i) Kariri _____

ii) Fariji _____

j) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kubadilisha nomino zilizopigiwa mstari kuwa vitenzi (ala. 2)
Wafanyikazi wote watafanyiwa tathmini ili kupata suluhu ya matatizo hayo.

k) Andika sentensi hii katika usemi halisi

(ala. 3)

Amina alikubali kuwa yeye ndiye mwizi aliyekuwa anawatatanisha wanakijiji.

l) Andika sentensi hii kwa ukubwa wingi

(ala. 2)

Kidudu hiki kimekiuma kitoto kwenye kijuso

m) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo

(ala. 1)

Mama ameeepua sufuria

n) Anisha shamirisho katika sentensi hii

(ala. 3)

Mgomba mrefu zaidi ulikatiwa ng'ombe hao kwa panga.

o) Onyesha virai vilivyo katika sentensi hii.

(ala. 2)

Yule mwanabiashara amepata hasara kubwa.

p) Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo (ala. 3)
Huyu ndiye mwalimu aliyekuwa akisomesha Kiswahili.

q) Tunga sentensi moja yenye vitate vifuatavyo (ala. 2)

i) Chati

ii) Shati

r) Tunga sentensi sahihi yenye kishazi tegemezi kama kivumishi (ala. 2)

ISIMU JAMII

1. A: Bwana asifiwe!

B: Amen.

A: Karibu ndugu mpenzi. Bwana akuita umfungulie moyo wako.

B: Nami naupokea mwito huo wa Bwana aliye juu.

MASWALI

a) Taja sajili ya mazungumzo haya (ala. 1)

b) Eleza sifa nne za sajili hii. (ala. 4)

2. Binadamu hutumia sauti kuwasiliana. Taja njia nyinginezo tano za mawasiliano. (ala. 5)

JINA _____ NAMBARI _____

DARASA _____ SAHIHI _____

TAREHE _____ SHULE _____

102/3

KIDATO CHA TATU

KARATASI YA TATU

FASIHI

JULAI : 2019

MUDA: SAA 2 1/2

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2019

(KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION)

Maagizo;

- Jibu maswali matatu pekee.
- Swali la kwanza ni la lazima
- Maswali hayo mengine mawili yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na fasihi simulizi.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
- Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

Kwa matumizi yam tahini pekee.

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
Jumla		

1. **SEHEMU A: USHAIRI (LAZIMA) (ALAMA 20)**

Soma shairi uliopewa kwa makini kasha ujibu maswali.

Mwenye macho wafishasha, wajiona kama ndovu
Kitu kimekuleweshwa, huutambuwi uovu,
Ngoma yako itakesha, au ni nguvu za povu.
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Tangu ukipate kitu, 'megeuka mpumbavu,
Kau hutuamini mtu, ambaye kwamba mtovu,
Wafikiri kisugutu, hakikati nyama pevu?
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Wangapi meonekana mibakhili mishupavu,
Walivyowakijitona, na wingi usuluhivu,
Leo hawana si tena, wageuki la maivu
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Kupata kusikughuri, ukajidhani mwerevu,
Wahichochako kiburi, wewe ni maangavu,
Iko siku itajiri, ujikute kwenye wavu
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Kila mwenye kukuonya, uiwatendi ya mbovu,
Huchelewi kumuvinya, kumvunda zake mbavu,
Fanya ambayo wafanya, hutajinyowa mashavu
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Maswali ya shairi

a) Weka shairi hili katika bahari tatu

alama 3

b) Fafanua toni ya mwandishi

alama 2

c) Eleza dhamira katika shairi hili

alama 2

d) Pambanua umbo la ubeti wa tatu

alama 3

e) Dhihirisha tamathali ya usemi iliyotumiwa katika molto wa ubeti wa pili

alama 2

f) Mwandishi ametumiaje uhuru wake?

alama 4

g) Uandike ubeti wa nne kwa lugha ya nathari

alama 4

SEHEMU B: Riwaya chozi la heri

Jibu swali la 2 au 3

2. Nimeonja shubiri ya kuwa mtegemezi kihali na mali.

Lakini katika yote hayo, nimejifunza mengi''

a) Eleza muktadha wa dondoo hili

alama 4

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

Soma mazungumzo yafuatayo kasha ujibu maswali

Mhusika A: Shikamoo

Mhusika B: Marhaba mume wangu.

Mhusika A: Mimi naona nikikutaliki

Mhusika B: (Akijaribu kufungia kicheko) Ukinitaliki utapikiwa na nani na naona magego yanaanza kukutoroka?

Mhusika A: (Akisafisha koo) Usidharau mke wangu. Haya si meno. Ni msumeno. Yaweza yakatafuna mifupa yako tebweretebwere.

Mhusika B: (Kwa umakini) Babu, nina swali.

Mhusika A: Uliza mpenzi

Mhusika B: Kwa nini una nywele nyingi kichwani kama kichaka chenye nyasi nyeupe?

Mhusika A: (Akitabasamu) Hizi huitwa mvi. Huwa ni mapambo. Ni chombo iliyotumika kumvutia bibi yake akakubali kufunga pingu za maisha name akijua bado barobaro.

Mhusika B: (Anashtuka) Naskia sauti ya mama ikiita. (Anatoka mbio)

Maswali

- a) Tambua kipera hiki cha mazungumzo (al 2)

- b) Fafanua sifa tano za kipera hiki (Al 5)

- c) Eleza kwa hoja tano ni kwa nini kipera hiki kinafaa kuhimizwa katika jamii ya sasa (Al. 5)

d) Eleza kwa hoja nne sababu zinazosababisha kufifia kwa kipera hiki katika karne hii (al 4)

e) Toa mifano minne ya ngomezi ya kisasa (al 4)

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2019

102/1

KIDATO CHA TATU

KISWAHILI

KARATASI YA KWANZA

INSHA

MWONGOZO WA INSHA

1)

JINA LA GAZETI	
MADA	TAREHE
JINA. MHARIRI	

Baadhi ya hoja

- a) Kupatikana kwa nafasi za ajira.
- b) Kupunguza msongamano wa magari ya abiria na hata yale yanayobeba mizigo.
- c) Ajali barabarani zitapungua
- d) Kuimarika kwa uchumi
- e) Bidhaa zenye uzani mzito kubebwa kwa urahisi na wepesi.
- f) Bei ya kusafisha bidhaa kuwa nafuu
- g) Kuongezeka na kukua kwa viwanda kutokana na usafirishaji wa bidhaa kwa bei nafuu na kwa haraka.
- h) Kupungua kwa uharibifu wa barabara utokanao na matumizi ya malori makubwa ya mizigo hivyo kupunguza gharama na ukarabati wa barabara.
- i) Kukua na kuendelea kwa kilimo nchini. Hii ni kutokana na usafirishaji wa mavuno sokoni pamoja na pembejeo kwa urahisi na kwa bei nafuu.
- j) Kuimarisha utalii nchini.

- 2)
 - i) Kuondoa uofisadi ili kukuza uchumi.
 - ii) Kuimarisha miundo msingi – vijana wataajiriwa.
 - iii) Kuanzisha viwanda
 - iv) Kutoa mikopo kwa vijana
 - v) Kuimarisha kilimo
 - vi) Kuboresha elimu.
 - vii) Kuhamasisha vijana kutochagua kazi
 - viii) Miaka ya kustaafu ipunguzwe
 - ix) Kukuza uchumi

- 3) akunyimaye mbaazi kakwepushia mashuzi
 - mwanafunzi ashughulikie pande mbili za methali.
 - Mwanafunzi aonyeshe waziwazi kuwa anayekudhibiti kufanya jambo fulani hukupunguzia kukabiliana na athari zitokanazo na jambo hilo.

- 4) Mwanafunzi atunge kisa cha kuisimua na athihirishe kishindo.
 - Maneno ya mdokezo yawe mwanzoni
 - Azingatie wahusika – halaiki na huyo anayewasili.
 - Miktadha mbalimbali kama vile; siasa, harusi, ziara ya rais.

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2019

102/2

KIDATO CHA TATU

KISWAHILI

KARATASI YA PILI

MWONGOZO WA LUGHA

Ufahamu

(alama 15)

- a) i) Tofauti za rangi
ii) Tofauti za kitamaduni
iii) Hali ya kiuchumi
iv) Uana / jinsia
- b) Hali ya watu wanavyoishi; tabia, mila na desturi zao, ustaarabu wao (hoja $1 \times 2 = 2$)
- c) Ubaguzi wa sasa upo kati ya matajiri na maskini. Wenye hali nzuri kiuchumi hujiona bora kuliko wali wa hali ya chini. (alama 2)
- d) i) Utamaduni wa kiafrika umengangia katika kumdhalalisha mwanamke nafasi yake ni pale jikoni.
ii) Taasubi za kiume.
iii) Dini- ambayo inamweleza mwanamke kuwa yuko chini yam me.
iv) Mwanamke hajajikomboa kimawazo. Anjiona hana uwezo/ni kiumbe dhaifu.
(hoja zozote $3 \times 1 = 3$)
- e) Nchi nyingi haziwezi kupiga hatua kimaendeleo. Husababisha migogoro/migongano miongoni mwa wanajamii/kutolewa kati ya wanajamii. (alama 2)
- f) i) Ubaguzi: Utengano unaotokana na sababu mbalimbali
ii) Masalia: Mabaki. (alama 2)
makosa:
Sarufi – usiondoe zaidi ya nusu ya alama alizopata katika kila kijisehemu.
Tahajia – Ondoa makosa 6 yaani alama 3 katika sehemu nzima ya ufahamu.

2) UFUPISHO

(ALAMA 15)

- a) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi? (alama 7, utiririko)
- Tunapinga na kulaani visa vya ugaidi.
 - Ugaidi ni kitendo cha kinyama kinachotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu.
 - Ugaidi hauna uhusiano na dini yoyote.
 - Polisi wanazembea katika kuzuia matendo ya kigaidi.
 - Polisi wabuni njia mbadala ya kukabiliana na ugaidi badala ya kunasa raia wasio na hatia.
 - Wakenya wasio na makosa huteswa na kuuawa kinyama.
 - Magaidi watalipia matendo yao.
 - Wakenya wana haki ya kulindwa kikatiba.
- Hoja zozote $7 \times 1 = 7$, alama ya utiririko

b) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50, fupisha aya mbili za mwisho, (alama 6, 1 utiririko)

- Raia wasio na hatia hunaswa
- Hurundikwa kwenye seli na kuachiliwa huru kama wameteseka.
- Huu ni ukiukaji wa haki za binadamu.
- Hii ni hila ya polisi kujionyesha kuwa wanafanya kazi.
- Magaidi huendeleza shughuli zao.
- Polisi wanapaswa kubuni njia zinazowapa mwelekeo mwafaka kuhusu wahalifu.
- Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo.
- Maafisa wa usalama kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

Hoja zozote $6 \times 1 = 1$, alama 1 ya utiritiko.

Ondoa $\frac{1}{2}$ alama kwa kila kosa la hijai hadi makosa sita kila litokeapo mara ya kwanza.

MWONGOZO (SARUFI)

a) i) (e)

ii) (gh) $2 \times \frac{1}{2}$ Al 1

b) Wa – O – a – o
Nafsi ya mzizi kiishio O rejeshi Al. 2

Tatu wingi

c) “Hivyo ndivyo tunavyoweza kufikia ‘Vision 2030’ Wewe waonaje?” $6 \times \frac{1}{2}$
Al. 3

d) M-mi mfano; mti – miti
(2×1) Al 2
Mw – mi mfano; mwavuli – miavuli

e) i) Choka – chokea 2×1 Al 2

ii) Ja – Jiwa

f) Mtoto wa Kamau alikuwa anapenda matunda
Kadiria sentensi ya mwanafunzi Al. 3
 $6 \times \frac{1}{2}$

g)

S				
KN		KT		
N	V	T	N	V
Mkufunzi	hodari	Amepita	Mtihani	rahisi
$6 \times \frac{1}{2}$				(al 3)

TB: hakikisha jedwali limefungwa.

h) Kusiko na njaa hakuhitaji msaada. (al 2)

i) i) Mkarara; ukariri

ii) Faraja; mfariji (2×1) Al. 2

j) wafanyakazi wote watatathminiwa ili kusuluhisha tusuluhishe matatizo hayo (Al. 2)

k) “Mimi ndiye mwizi ninayewatatanisha wanakijiji,” Amina alikiri

l) Madudu / majidudu haya yameyauma matoto / majitoto kwenye majuso. Al 2

m) Mama amejika sufuria Al 1

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2019

102/3

KIDATO CHA TATU

KISWAHILI

KARATASI YA TATU

FASIHI

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. a) i) Tarbia - lina mishono minne kila ubeti
ii) Ukara – vina vya mwisho vinatiririka
iii) Mathnawi – Lina migao miwili
- b) Toni ya mshairi ni ya masuto na maonyo $2 \times 1 = \text{Al } 2$
- c) Dhamira ya shairi kukashifu/kusuta walionavyo wasiothamini wengine wenzao $2 \times 1 = \text{al. } 2$
- d) Una mishororo minne
- Una vipande 2 (ukwapi na utao) = katika kila mshororo.
- Kila mshororo una mizani 16 (8,8).
Vina na vu
 na vu
 na vu
 vu we
 $4 \times 1 = \text{al } 4$
- e) Jazanda – ‘kisu gutu’ $1 \times 2 = \text{al. } 2$
- f) Inkisari – Km ‘meonekana, megeuka’nk
Lahaja – km. Ndiya – jia
Maivu-yaloiva
Mazda KM. muwervevu
Tabidila. Km-ujuwe, waliyo, akajinyowa mwervevu $3 \times 1 = \text{al. } 3$
- g) Kutajirika kusipumbaze ukafikiri kuwa una maarifa sana, kuringa kwako ndiko kutakuangamiza.
- Wakati utafika ambapo utapatwo na hali ngumu usioweza kujinsua
- Hat mtu awe na maarifa au uwezo hajitoshelezi kwa kila kitu. $\text{Al. } 4$

RIWAYA – CHOZI LA HERI

2. “Nimeonja shubiri ya kuwa mtegemezi kihali na mali. Lakini katika yote hayo, nimejifunza mengi”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili $\text{Al } 4$
- Haya ni maneno ya Ridhaa
- Anamwambia Mwangeka
- Wamo katika ganjo la nyumba yao iliyochomwa.
- Anamweleza dhiki ambazo amepitia tangu ghasia za baada ya kutawazwa kiongozi mpya.
 $(4 \times 1 = 4)$
- b) Bainisha tamathali ya usemi inayojitokeza katika kauli hii (alama 21)
Msemu / nahau – onja shubiri
- c) Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari kwa kuyarejelea maisha ya mzungumzaji.
i. Kubomolewa nyumba
ii. Kutupeliwa – Anauziwa ardhi iliyotengewa ujenzi wa barabara
iii. Jengo lake la kibiashara linachomeka kutokana na hitilafu ya umeme.

- iv. Mzee Kendi anaichoma familia yake
- v. Nduguye Makaa anachomeka katika mkasa wa moto
- vi. Kuitwa mfuata mvua akiwa shuleni na wanafunzi wenzako
- vii. Kutengwa mchezoni – anatengwa mchezoni wakiwa shuleni.
- viii. Kusimangwa – wanafunzi wenzake kumdhihaki na kumsimanga
- ix. Kusingiziwa wizi – wanafunzi wenzake wanamsingizia kuwaibia
- x. Kubakwa kwa wapwewe – Lime na Mwanaheri wanabakwa
- xi. Kukatwa kwa dadake – subira anakatwa na wahuni
- xii. Kula mzizi mwitu – anakosa chakula kambini na kulala mizizi mwitu
- xiii. Kuugua – anaugua shirikizo la damu
- xiv. Anaishi maisha ya upweke baada ya mkewe kuaga
- xv. Kitindamimba wake Dede alifariki akiwa na umri wa miaka sita.
- xvi. Alizaliwa katika ndoa ya mitora – babake alikuwa na wake kumi na wawili.

(14x1)

3) Wanawake katika “chozi la heri” ni mawakala wakuu wa ukiukaji wa haki za binadamu”.

Thibitisha.

Alama 20

- i. Mama Pete onamkatiza mwanawe pete masomo kwa kumuoza kwa mzee fungo. Akiwa darasa la saba
- ii. Mama Pete anamtelekeza pete kwa nyanyake bila kutuma mahitaji muhimu.
- iii. Mama Sauna anadhulumu mwanawe Sauna kwa kumuonya dhidi ya kumwambia yeyote jinsi babake amekuwa akimbaka.
- iv. Mama Sauna anakiavya kijusi cha Sauna baada ya kupachikwa mimba na babake.
- v. Sauna anawaiba Dick na Mwaliko na kuwapeleka kwa Bi Kangora anayefanya biashara haramu ya kuwauza watoto.
- vi. Bi Kangara anawauza wasichana walioibwa na mawakala wake madanguroni ili watumike kama vyombo mapenzi.
- vii. Mama Kaizari anamdhulumu Subira kwa sababu ya tofauti zao za kiusuli. Wanamwita Muki.
- viii. Tuama anayeunga mkono upashaji tohara wa wasichana licha ya tohara hiyo kuwaua wasichana wengi.
- ix. Satua anamdhulumu Chandachema baada ya kuhamia nyumbani kwake.
- x. Annete anawaita wanawake waliofanya kazi nyumbani mwake vimodo wa mumewe kiriri.
- xi. Tindi anampeleka nduguye Lemi klabuni na kucheza densi hadi alfariji bila kuwazia kwamba Lemi anahitaji kula kutokana na uchovu.
- xii. Zohali anakataa kumfahamisha mwanawe Nasibu kwamba ana babu na nyonya kwa sababu ya dhuluma walizomtendea wazazi wake.
- xiii. Wanawake wanafanya ukahaba na Tenge Bi. Kimai anapoenda kazini.
- xiv. Wanawake wanajifungua watoto na kuwatupa jaani kama motto aliyeokotwa na neema.
- xv. Rehema anamzaa Chandachema na kumwacha na babake fumba na kutowahi kurudi kumjulia hali.
- xvi. Kiongozi katili – visakale vya majirani
- xvii. Mamake zohali anadhulumu mwanawe akiwa mja mzito.
- xviii. Annete, Subira na Naomi kuacha familia zao bila kujali.
- xix. Wanawake huwapiga waume – Mamia ya wanaume wanapigwa bila ya kupata wa kuwatetea.
- xx. Wanawake huwanyima waume zao haki za unyumba. Hii inaedelea dhiki za kisaikolojia

(zozote 20 x 1 = 20)

TAMTHILIA – KIGOGO

- 4) "...kwa tamaa mtu....amepanda kufikia kilele cha ufanisi kwa kukanyaga migongo ya wenziwe."
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili alama 4
ni maneno ya Babu
Anamwambia Majoka
Wamo kwenye chumba cha wagonjwa
Babu anazunguza na majoka akiwa usingizini akimsuta kwa kuwadhulumu raia anaowaongoza.
 $4 \times 1 = 4$
- b) Bainisha tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 4)
- i. Jazanda – kukanyaga migongo ya wenziwe.
ii. Taswira – picha ya mtu anayeikanyaga migongo ya wenziwe
 $(2 \times 2 = 4)$
- c) Huku ukitumia hoja kumi na mbili onyesha jinsi anayeambiwa maneno haya alivyowakanyaga wenzake migongo katika kufikia kilele cha ufunisi wake. Al 12
- i. Mauaji – anamuua Jabali kiongozi wa chama cha mwenge ili kupunguza upinzani wa kisiasa dhidi yake, hivyo kuendelea kuongoza jimbo la sogamoyo.
ii. Kupandisha bei. Anapandisha bei ya chakula maradufu ili kupata faida bila kufikiria maisha ya raia maskini aliowaongoza.
iii. Kodi – anapandisha kodi hivyo kuwasababisha wafanyakazi kama vile walimu na wauguzi hulipwa mshahara duni na serikali kupata kodi kubea.
iv. Mshahara duni. Anawalipa walimu na wauguzi mshahara duni.
v. Kemikali – anamwaga kemikali na taka za kiwanda chake katika soko la chapakazi.
vi. Hongo – serikali yake inaitisha hongo kutoka kwa wanabiashara inapokusanya kodi sokoni chapakazi.
vii. Ukame – amefungulia biashara ya ukataji miti hali inayofanya mvua kutonyesha.
viii. Kuwavamia raia – anawatuma wahuni kumvamia Tunu na kuumumiza mguu kupinga uongozi wake dhalimu.
ix. Deni – Anatumia ufadhili kutoka mataifa ya nje kugharimia uchongoji wa kinyago cha babuye na kisha raia kulipa deni hilo miaka mia moja.
x. Kufunga soko – analifunga soko lililokuwa tegemeo la raia ili kujenga hoteli yake hivyo kuwasababishia raia kutoabika.
xi. Ukabila – anasambaratisha umoja wa jamii za sagamoyo kwa kusambaza vikaratasi kabila moja kuhama.
xii. Kugunga raia. Anamfunga Ashua ili amlazimishe mumewe Sudi kumchongea kinyongo.
xiii. Kufunga runinga. Anafunga runinga ya mzalendo ili raia wasiopata kuona maandamano yanayoendelea.
xiv. Kubomoa vibanda – anabomoa vioski vya wanabiashara sokoni chapakazi ili ajenge hotel yako.

(Za kwanza $12 \times 1 = 12$)

- 5) "Majoka anatumia mbinu namna kwa namna kujizatiti uongozini" Thibitisha.
- i. Mauaji – Majoka alimuua Jabali
ii. Vitisho – uk. 11 Kenga anamtisha Sudi.
iii. Kutoa misaada mf. Ya chakula kwa wale wasiojiweza uk.6
iv. Kuangamiza upinzani – Tunu anaumizwa
v. Maskinisha raia – Majoka kufunga soko.
vi. Hongo – atakayechonga kinyongo cha majoka atatunukiwa uk.11

- vii. Kuvunja sheria – kumkubali Asiya kuuza pombe
- Ukataji wa miti.
- viii. Kudhibiti vyombo vya habari – runinga ya mzalendo inafungwa.
- ix) Vyombo vya dola – polisi wanatumia kutimua waandamanaji.
- x. Wapinzani kutiwa mbaroni – Ashua.
- xi. Raia kufurushwa katika maeneo Fulani ya nchi.
- xii. Kuharamisha maandamano – Ashua
- xiii. Propaganda – Majoka kusifu sagamoyo redioni.
- xiv. Tuzo/vishawishi – Sudi anaahidiwa tuzo na zawadi nyinginezo ili kuchonga kinyago.
- xv. Vikaragosi – mshauri mkuu Kenga, askari.
- xvi. Unsaba – uongozi unarithishwa kifamilia. Majoka ni mwanawe wa kiongozi Ngao Junior.
- xvii. Jela – intumiwa kulipiza kisasi na kuwatisha wazalendo K.V Ashua.
- xviii. Uchochezi – Wanaopinga mrengo tawala wanatupiiwa vijikaratasi vya kuwataka waondoke wanakoishi.
- xix. Hofu – Hashima anasema wanaishi kwa hofu.
- xx. Kuidhinisha shughuli haramu – upikaji wa pombe haramu na ukataji wa miti.
- xxi. Matumizi ya misimbo – majoka na Kenga wantumia lugha ya kitamathali au msimbo k.m kuvunja mguu – kuua.
- xxii. Kutoa ajira kwa watu wao – kenga ni binamu wa majoka.
- xxiii. Ukiritimba – lengo la majoka ni kuwa na chama kimoja cha kisiasa, kampuni zinazotajwa kwa majina.

(Zozote 20 x 1 = 20)

HADITHI FUPI

A. CHOKOCHO NA KAYANDA” TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

6.Kile kile ambacho kuta zake zilishuhudia kwa macho yake ndoa yake ndoa yetu ikifungwa.

...Kazi yetu kubwa ni ya kijungu meko, kazi ya kupigaia tumbo....

a) Eleza muktadha wa dondoo hili al.4

- Mzungumzaji ni mashaka
- Anarejelea makazi duni anamoishi na familia yake.
- Ndoa anayorejelea kwa urejeshi ni kati yake na waridi aliyeshurutishwa kuoa.
- Amezungukwa na (yeye na aila yake) umaskini wa kila nui.
- Hali yao ya sasa imesababisha na kulazimishwa kuoa waridi bila mpango kama huo.
- Hali hii inasababisha kutoka katika familia/kuondoka kwa wandi pamoja na watoto wake.

4x1

b) Onyesha tamathali mbili zinazojitokeza katika mukuzi huu Al. 2

uhushi – kuta zilishuhudia

usemi – kazi ya kijungu meko 2x1

c) Fafanua sifa sita za mhusika anayezungumza katika muktadha huu. (ataje mzungumzaji) Taabiri

mpenda amani

makunifu

mvumilivu

msalihina

mwenye majuto

mkulima

yatima

mfanyakazi

Hoja sita na maelezo (al.1)

6x1

d) Kwa ufafanuzi onyesha dhiki anazopitia msimulizi wa hadithi hii (a15)

- Yatima / uyatima baada ya kufa kwa wazazi wake
- Kufa kwa mamake mlezi Biti Kidebe.
- Maradhi kwa Biti kidebe yaliulazimu kumlea mama yake akiwa na umri mdogo.
- Kulazimishwa na mzee Rubeya Waridi – akiwa hajapanga.
- Kuzaa watoto wengi (saba) kwa kipindi kifupi kwani walizaliwa pacha mara tatu kasha moja
- Okesefu wa ajira mwafaka ambayo ingemwezesha mashaka kuikimu familia yake.
- Chumba kidogo ambapo ilimbidi kunyenyekea kwa chakupewa ili wavulana wapate pa kulala jikoni mwake.
- Kazi ya ulinzi katika kampuni ya zuia wizi security (ZWS) ili mnyima fursa ya kutangamana na familia usiku.
- Kutoweka / kuondoka kwa Waridi na watoto kulimletea dhiki zaidi
- Kukosa pesa kunamfanya ahisi kuwa hana uwezo wa kumkabili mkewe Waridi kwani pesa ni kila kitu kwa jamii ya kisasa.

(mwalimu akidirie hoja)

(8x1)

7) (i) Safia – Shogake dada ana ndefu

Alijiingiza katika mapenzi kiholela akawa mjamzito

Aliavya mimba akaaga

ii. Bi. Hajmida na Bw. Masudi

Walimruhusu safia asaidiwe kudurusu na

kimwana, akaringwa – wakaainika

iii. Oti – Nizikeneni papa hapa

Alijuana na Wanjiru akaambukizwa ukimwi akafa

iv. Mkubwa – mkubwa

Ndotoni aliwaona wanawe wa kiume wakitumia dawa za kulevya – alizokuwa akiuza.

v. Dadi – Masharti ya kisiasa

Analalamikia masharti ambayo lazima ayatimize

Ilhali aliyakubali ili amuo kidawa

vi. Dennis – mapenzi ya kifaurongo

Amebukuzwa na Penina ilhali alimkubali awe mpenziwe.

vii. Samueli – Mtihani wa maisha

Alifeli mtihani kwa kuwa hakutilia masomo maanani

viii. Mkumbukwa – mkubwa

Alifungwa kwa kuuza dawa za kulevya.

ix. Penina – mapenzi ya kifaurongo

Mapenzi yake na Dennis hayakudumu

x. Wanjiru – nizikeneni papa hapa

Aliambukizwa ukimwi

xi. Jairo – Mwalimu mstaafu

Alimpokeza mke na wanawe Mosi halafu analalamika kuwa bintiye ameolewa na Mosi.

xii. Wanakamati wa chama cha nyumbani –

Nizikeneni papa hapa

Walikataa ushauri wa Oti – baada ya ajali walimzika alipotaka

Tanbihi – Mtahiniwa lazima afanye hadithi.

(10 x 2)

8) FASIHI SIMULIZI**(SEHEMU YA E)**

- (a) Malumbano ya utani. Babu anamtania mjukuu wake kwamba angemtaliki kana kwamba alikiwa mke wake. (2x1)
- (b) (i) Hufanyika kati ya watu wenye uhusiano mzuri kama vile mababu.
ii) Husheheni mizaha ambayo hailengi kuudhi
iii) Utani huwa na mipaka Fulani
iv) Mbinu ya chuku hutumiwa kwa mapana
v) Hufanyika baina ya watu wawili au makundi mawili.
vi) Hutumia lugha ya kisanii ama kiufundi
(5 x 1)
- c) Huimarisha uhusiano mwema baina ya watani
hupunguza urasmi ambao huwepo baina ya wanajamii wengi.
Hukosoa hueka zisizofaa kwa kuzidhihaki
Hutumika kupitisha muda
Hutambulisha jamii
Huzua burudani
(5 x 1)
- d) Mitindo mipya ya maisha hivi kwamba wanajamii huhamia kwingineko na kutangamana na wanajamii wengine.
- Baadhi ya vijana hupuuza mababu na mabibi kwa kuwaona kama wasioelimika.
- Ukosefu wa utafiti wa kutosha hivi kwamba ni machache sana yanayofahamika katika jamii ya sasa.
- Maendeleo ya kiteknolojia na sayansi
- Sera na uchochezi wa kisiasa.
4x1
- e) Kengele shuleni
Kipenga uwanjani
Honi za magari
Binja
Ving'ora
Milio ya Abulensi
4x1